# DHAMIRA

Idara ya Afya ya Umma ya kaunti ya Winnebago inajikita katika kuimarisha na kuhamasisha afya ya jamii kwa kutoa huduma bora, kushirikiana kwa umakini, na kutekeleza mbinu pamoja na sera za haki ili kuhakikisha maisha bora kwa kila mmoja.





Idara yetu ya Afya ya Umma ina wataalamu waliobobea katika kuimarisha afya ya jamii. Tunashirikiana na majirani zetu pamoja na mashirika mengine ya kijamii katika kushughulikia changamoto kubwa zinazojitokeza, ili kuhakikisha kuwa Kaunti ya Winnebago inastawi kwa vizazi vijavyo.

## WASILIANA NASI

**Tupigie simu bure: 1-800-250-3110**

**Barua pepe: health@winnebagocountywi.gov**

**Tovuti: www.winnebagocountywi.gov/health**

**facebook.com/WinnebagoHealth**

## VITUO VYETU VINAPATIKANA KATIKA MAENEO YA OSHKOSH NA NEENAH:

### OSHKOSH

112 Otter Ave,
Oshkosh

**Simu:** 920-232-3000

**Simu ya kuwasiliana na WIC:** 920-232-3350

**Faksi:** 920-232-3370

### NEENAH

211 N Commercial St, Neenah

**Simu:** 920-727-2894

**Simu ya kuwasiliana na WIC:** 920-729-2945

**Faksi:** 920-729-2972

**Vituo vyetu vyote viko wazi kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 10:30 jioni, siku za Jumatatu hadi Ijumaa.**

Public Health
Prevent. Promote. Protect.
Winnebago County, WI

winnebagocountywi.gov/health

*Zuia. Hamasisha. Linda.*

Public Health
Prevent. Promote. Protect.
Winnebago County, WI



# KWA PAMOJA, TUNAWEKEZA JUHUDI KATIKA KUJENGA JAMII YENYE AFYA BORA

# HUDUMA ZETU

## AFYA YA FAMILIA

**Programu ya rasilimali kwa wazazi**

- Uchunguzi wa Maendeleo
- Ukaguzi wa Usalama wa Viti vya Magari*
- Msaada wa Kunyonyesha
- Kituo cha Kujitolea Maziwa ya Mama
- Chanjo kwa Watoto*
- Usingizi Salama
- Upimaji wa Madini ya Risasi kwa Watoto

**Programu ya Fit Families**

*Umri na kipato vinazingatiwa

**WIC (Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto Wakubwa)**

WIC ni mpango wa virutubisho mbadala vya lishe unaolenga watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano pamoja na akina mama wajawazito, wanaonyonyesha, au waliojifungua wenye kipato cha chini hadi cha wastani. Huduma zinazotolewa ni pamoja na:

- Msaada wa Virutubisho Mbadala vya Lishe
- Elimu na Ushauri kuhusu Lishe
- Msaada wa Kunyonyesha
- Programu ya Fit Families
- Kuponi za Programu ya Farmer's Market



## AFYA YA MTU BINAFSI

Programu ya Wisconsin Well Woman

Huduma za afya za bure kwa wanawake wenye bima ya afya ndogo au wasio na bima kabisa, kama vile:

- Uchunguzi wa Matiti pamoja na Afya ya Uzazi
- Mammogram (uchunguzi wa saratani ya matiti)
- Uchunguzi na vipimo maalum, kama vile ultrasound na biopsy
- Vipimo vya Pap (uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi)
- Uchunguzi wa Virusi vya Papiloma ya Binadamu (HPV)

Kupunguza Madhara

Huduma hizi ni za siri na hazitambulishi watu kwa majina, na zinajumuisha:

- Narcan na jinsi ya kuitumia
- Sanduku za kuhifadhi dawa ambazo hazihitajiki tena
- Huduma za Upatikanaji wa Sindano za LifePoint
- Vipimo vya Fentanyl
- Upimaji wa Virusi vya Ukimwi na Homa ya ini (Hepatitis C)
- Huduma ya kuunganishwa kupata matibabu
- Mashine za Utoaji wa Huduma za Afya ya Umma

## UZEE WENYE AFYA

**Vipindi vya Wellness Plus**

**Tathmini ya Hatari ya Kuanguka – nyumbani!**

**Kupata Usawa Pamoja**

*** Huduma zilizoorodheshwa ni baadhi tu ya huduma zinazopatikana ***

*Wasiliana nasi ili kupanga miadi kwa kupiga simu kupitia (920) 232-3000

**Tupigie simu ili kufahamu kama unakidhi vigezo

## AFYA YA MAZINGIRA

**Udhibiti wa athari zinazotokana na Madini ya Risasi**

- Uchunguzi wa Madini ya Risasi kwa Watoto
- Mpango wa Nyumba Salama bila Madini ya Risasi(LeadSafe): Inajikita katika kutoa huduma za kuondoa madini ya risasi kwenye nyumba zinazokidhi vigezo, pamoja na kwenye nyumba za kupanga

**Upimaji wa Ubora wa Maji**

- Maji ya Kunywa
- Fukwe za bahari
- Mabwawa ya kuogelea

**Vifaa vya Upimaji wa Radon**

**Leseni, Vibali na Ukaguzi**

**Huduma za Wanyama**

- Majeraha yanayotokana na kung'atwa na mnyama
- Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa

## AFYA YA JAMII

**Ushauri Nasaha na Ufuatiliaji wa Magonjwa ya Kuambukiza**

**Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa Yanayoambukizwa kwa Njia ya Kujamiiana**

**Chanjo**

**Ushauri Nasaha na Upimaji wa Virusi vya Ukimwi na Homa ya ini (Hepatitis C)**

**Elimu ya Kukabiliana na Hali Mbaya ya Hewa**

**Programu ya Kupunguza Madhara**



*Zuia. Hamasisha. Linda.*